Tuko Katika Biashara Gani?

(Which Business Are We In?)

na

Ellis P. Forsman

Tuko Katika Biashara Gani?

(What Business Are We In?)

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Tuko Katika Biashara Gani?

Mat. 16:21-23

Ndege ya kampuni ya Eastern yenye namba 401 ilikuwa inakwenda Florida mnamo Disemba 29, 1972, na ilikuwa na zaidi ya watu 200 ndani.

Wakati ikiwa inaendelea na safari mwanga mdogo ukaonekana (kwenye tairi ya mbele ambayo ndio gia ya kusimamia). Injinia wa ndege akaiona na akaanza kuuliza maswali. Kwa vile kila kitu sehemu zingine kilikuwa sawa, akaona kwamba ni balbu ndiyo ilikuwa inaungua. Hivyo akaamua kuitoa na kuweka nyingine.

Akapata shida na akamuomba rubani msaidizi ili amsaidie. Rubani alihairisha kutua, na akainua ndege hadi kiwango cha mita 2000, na akaanza kuzungusha ndege angani hadi walipo maliza kutatua tatizo. Wawili hao wakiwa wanafanya kazi pamoja hawakuweza kubadilisha balbu, hivyo rubani akaiweka ndege katika urubani wa kujiendesha yenyewe na akaja kusaidia. Kila mmoja alikuwa na wazo lake mwenyewe jinsi ya kulitatua tatizo na mjadala wa hali ya juu ukaibuka miongoni mwao. Lakini walipaswa kuweka balbu mpya.

Hivyo, ndege ilikuwa inashuka. Mtazamo wa nahodha ulikuwa katika balbu ambayo haina gharaama, wakati ndege yenye gharama na watu 2000 walikufa ndege ilipoanguka ikiwaangamiza wote.

Petro pia, alikuwa na tatizo la kutoka nje ya msitari.

Mat. 16:21-23, "*Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka. Petro akamchukua akaanza kumkemea, akisema hasha Bwana hayo hayatakupata. Akageuka akamwambia Petro, nenda nyuma yangu shetani; u kikwazo kwangu; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.*"

Si ungechukia kuitwa "Shetani" na Mwana wa Mungu?

Lakini mtazamo wa Petro ulikuwa wa ubinafsi na kutokuwa mahali pake.

2 Tim. 2:4, "*Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari.*"

Tuko Katika Biashara Gani?

Jinsi tunavyotembea katika gwaride: hii ndiyo biashara yetu!

- Mat. 28:19-20, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*"
- Marko 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*"

Sababu za kufanya uinjilisti

Kufuata mfano wa Kristo.

- Luka 19:10, "*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.*"
- Yoh. 3:16-17, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.*"
- 1 Tim. 1:15, "*Ni neon la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kaabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi.*"
- Yoh. 20:21, "*Basi Yesu akawaambia tena, amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi.*"

Yesu alishughulika na watu yeye binafsi.

Nikodemo. Yoh. 3:3, "*...mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.*"

Mwanamke kisimani. Yoh.4:25-26, "*Yule mwanamke akamwambia najua ya kuwa yuaja Masihi, (aitwaye Kristo); naye atakapokuja yeye atatufunulia mambo yote. Yesu akamwambia, mimi ninayesema nawe ndiye.*"

Zakayo. Luka 19:5, "*Na Yesu alipofika mahali pale alitazama juu, akamwambia Zakayo shuka upesi, kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako.*"

Kutimiza hitaji la ulimwengu

Kuna watu wanaodhani kwamba kila mtu ataokolewa.

- Mat. 7:13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.*"
- Yoh. 3:18, "*Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.*"

Jehanamu siyo somo maarufu Marekani leo, lakini hatuwezi kukwepa uhalisia wake – kuikataa hakutaifanya itoweke!

Yesu aliliongelea Jehanamu na akawaonya watu kuhusu hatari ya kwenda pale.

Mtu anaweza kupendekeza kwamba haipendezi kuongelea jehanamu, lakini inapendeza kuonya kuhusu hatari – ambacho haipendezi ni kufahamu hatari na kukaa kimya kuhusu jahanamu!

Ufu. 20:15, "*Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.*"

Yesu aliulilia Yerusalem, kwa sababu watu hawakumkubali.

Mat. 23:37-38, "*Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chingi ya mabawa yake, lakini hamkutaka! Angalieni nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa.*"

Paulo alichukizwa na Athene.

Mdo. 17:16, "*Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulvyojaa sanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake.*"

Watu wasio Mungu hushurutishwa, hawana msaada, huuzunisha na kukatisha tamaa. Hawana tumaini na wamepotea vibaya dhambini.

Dhambi inaharibu nchi yetu, mji na miji zetu. Inachana miji na maisha yetu yanakuwa mabaya zaidi.

Damu ya Yesu na injili ndiyo wokovu wetu pekee!

- Mdo. 2:40, "*Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi.*"
- Gal. 1:4, "*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu Baba yetu.*"

Hatupaswi kumtarajia mtu apate dhoruba katika maisha.

- Kupoteza unyayo, macho.
- Kupoteza kazi.
- Kupoteza nyumba.
- Kupoteza wapendwa wetu.

Kukaa katika umilele jehanamu ni mbaya kuliko vitu hivi vyote.

Kutimiza Ushurutisho Wetu Wa Ndani

Makuhaani walipowaamuru mitume kuacha kulihubiri jina la Yesu, walisema:

Mdo. 4:19-20, "*Petro na Yohana wakawajibu wakawaambia, kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe; maana sisi hatuwezi kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia.*"

Kama mwanamke aliyevalishwa pete ya uchumba ni vigumu kunyamaza.

Kama wenza wachanga wanaotarajia kupata mtoto, ni vigumu kunyamaza.

- 2 Kor. 5:14-15, "*Maana upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao.*"
- Rum. 1:14-16, "*Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima. Kwa hiyo kwa upande wangu mimi, ni tayari kuihubiri Injili hata na kwenu ninyi mnaokaa Rumi. Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.*"

Niko chini majukumu. Nina shauku. Sina aibu.

Mdo. 20:24, "*Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habari njema ya neema ya Mungu.*"

Kuwafanya Wanafunzi

Siyo kwamba Mungu anatutaka kufundisha na kutoka nje, bali anawataka wanafunzi.

Wanafunzi ni watu wanaomfuata Yesu na wanapendezwa kuwafundisha wengine nao wafanye hivyo.

Je wewe ni mwanafunzi? Aliyekomaa, anayewajibika, anayetoa wafuasi!

Kama ungekuwa na rafiki aliyehitaji kufanyika Mkristo, je unaweza kumfundisha?

2 Tim. 2:2, "*Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.*"

Hitimisho

Je Yesu anaweza kukuhesabia?

Je vizazi vijavyo vinaweza kujua ukweli? Watoto wetu watamfuata Yesu?

Majirani zetu wanaweza kujua kwamba tunampenda Bwana na kumtumikia?

Je waweza kuwa na muda kwa ajili ya Bwana?

Je unaweza kwenda mbinguni ukifa?